



FAIR COMPETITION COMMISSION



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA KUZINDUA BARAZA
LA WAFANYAKAZI LA TUME YA USHINDANI TAREHE 11
SEPTEMBER, 2013**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dk. Abdallah O. Kigoda (MB), Jumatano Novemba 11, 2013 anatarajiwa kuzindua Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Ushindani katika Ofisi za Tume ya Ushindani, zilizopo katika ghorofa ya pili, jengo la Ubungo Plaza majira ya saa tatu na nusu asubuhi.

Baraza hilo linaloundwa kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya Kanuni ya Majadiliano ya Pamoja ya Utumishi wa Umma Na 19 ya mwaka 2005 na kwa muundo wa uongozi wa tume ya Ushindani litakuwa na wajumbe wasioipungua 20 wakiwemo Mkurugenzi Mkuu, Wakurugenzi wa Idara, Mkuu wa Kitengo cha Utawala na Rasilimali Watu wa Tume, Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi la TUGHE, Mjumbe wa kuteuliwa kutoka Mkoa/Makao Makuu ya TUGHE, Mjumbe wa kuteuliwa na TUGHE Taifa kutoka Baraza kuu la Wafanyakazi Serikalini, Wajumbe wa kuchaguliwa na wafanyakazi toka kila Kurugenzi na Afisa Sheria wa Tume.

Hafu hiyo ya uzinduzi pia itahudhuriwa na makamishna wa Tume wakiwemo Kanali (Mstaafu) Abihudi Nalingigwa, Bibi Hilda Itika Mafwenga na Bibi Blandina Selle Gogadi. Wengine watakaohudhuria hafla hiyo ni pamoja na wawakilishi wa TUGHE Taifa, TUGHE Mkoa, Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro Mahala pa Kazi cha Mahakama Kuu (CMA), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na waandishi wa habari.

Baraza la Wafanyakazi la Tume linatarajiwa Iktekeleza majukumu ya kuongeza ufanisi wa utendaji wa shughuli za tume lakini hususan majukumu yafatayo kwa mujibu wa kanuni ya 30 ya kanuni ya Majadiliano ya Pamoja ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2005:-

- (a) Kuwashirikisha wafanyakazi katika utekelezaji wa shughuli za Tume ya Ushindani kama zilivyoanishwa katika Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 kwa ushirikiano na uongozi.
- (b) Kuishauri Tume ya Ushindani juu ya ufanisi wa kazi na hatua zinazofaa kuchukuliwa, kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo na Tume ya Ushindani ni za kuridhisha na zimo katika malengo yale.
- (c) Kuishauri Tume ya Ushindani juu ya mambo mengine muhimu yanayohusu maslahi ya wafanyakazi.
- (d) Kuishauri Tume ya Ushindani juu ya utaratibu wa kupandisha vyeo, motisha na nidhamu kwa wafanyakazi wa Tume ya Ushindani.
- (e) Kupokea, kujadili na kuthibitisha mipango na makisio ya mapato na matumizi ya Tume ya Ushindani.
- (f) Kujadili na kutoa ushauri juu wa mipango ya uendelezaji wa rasilimali watu katika Tume ya Ushindani.
- (g) Kuishauri Tume ya Ushindani (Bodi ya Tume) juu ya mipango na maendeleo ya Tume ya Ushindani.

Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Umma

Jumanne, Septemba 10, 2013.

Tume ya Ushindani, Ghor ya Pili, Ubungo Plaza, Morogoro Road,
P.O.BOX 7883, Dar es Salaam.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ndg. **Frank S. Mdimi, Afisa Mwandamizi,**
Mawasiliano na Mahusiano ya Umma kwa simu:+255222461565, 2461566, 2461568,
2461569; FAX:+255 222461567;Kiganjani: +255784762437 na +25573944083,B-Pepe:
info@competition.or.tz.